

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

WANANCHI WAFURIKA KUPIMA AFYA BURE VIWANJA VYA MNAZI MMOJA

Zoezi la Upimaji wa Afya Bure limeanza leo kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja huku baadhi ya Wananchi wakitoka Mikoani kuja Dar es Salaam kufuata huduma na wengine wakiwahi kwenye Viwanja hivyo tokea saa 10 Alfajiri.

RC Makonda amesema kampeni hiyo ina malengo matatu ambayo ni÷

- Kujengea Wananchi utaratibu wa kupima Afya zao mara kwa mara hata kama hawaumwi.
- Kusaidia wananchi Wanyonge wanaotamani kupima Afya lakini hawana Uwezo wa Fedha ili kupata fursa ya kupima Afya.
- Kupunguza vifo vitokanavyo na watu kutokujua historia ya Magonjwa yao hadi pale wanapougua.

Aidha Makonda amesema kila Mwananchi atakaefika kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja atapimwa na kupatiwa Matibabu Bure.

Amesema Wananchi wengi wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na kukosa utaratibu wa kupima Afya mara kwa mara na pindi wanapozidiwa na kufikishwa Hospitali ugonjwa unakuwa tayari umekuwa sugu hivyo kupoteza maisha.

Amewapongeza Madaktari na Wauguzi kutoka Hospital za Umma, Jeshi na zile za Binafsi kwa kujitolea kumuunga mkono katika Kampeni hiyo.

Zoezi la upimaji Afya Bure litaendelea Kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja kwa muda wa siku **tano kuanzia Asubuhi hadi Jioni**.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

06/08/2017